

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



OFISI YA MKUU WA WILAYA YA NYANG'HWALE

NGL/S.1/1/VOL.1/48

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyang'hwale anakaribisha maombi ya kazi za mashariti ya muda kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi zifuatazo: -

1.0 MWANDISHI MWEENDESHA OFISI (KATIBU MAHSUSI). NAFASI

MBILI (02).

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

- Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye stahhada (Diploma) au cheti cha NTA level 6 ya uhazili.
- Awe amefaulu masomo ya hati mkato ya Kiswahili na kingereza maneno 100 kwa dakika moja na awe amepata Mafunzo ya Compyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Window Microsoft office, Internet, Powerpoint, e – mail na Publisher.

1.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na za siri.
- Kupokea wageni na kuwaelekeza wanapoweza kutatuliwa shida zao.
- Kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio mbalimbali ya ofisi.
- Kutunza majalada, kuyagawa kwa maofisa kwenye ofisi ili nyaraka za maelekezo zishughulikiwe kisha kuyakusanya baada ya kufanyiwa kazi na kuyatunza.
- Kusambaza barua na nyaraka mbalimbali kwenye taasisi zingine na mahali atakapotumwa.
- Kufanya usafi ndani na nje ya ofisi.

- Kuandaa chai/Chakula cha watumishi wa ofisi.
- Kutekeleza kazi zote atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

1.3 MLINZI WA OFISI NAFASI MOJA (01).

1.4 SIFA ZA MWOMBAJI.

- Kuajiriwa aliyemaliza elimu ya Kidato cha nne aliyefanya Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Akiba.
- Awe na afya njema
- Hajawahi kupatikana na hatia na kutumikia kifungo.
- Awe mtanzania.

MASHARITI YA JUMLA.

- Mwombaji awe mtanzania asiyezidi umri wa miaka 45
- Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika utumishi wa umma.
- Hajawahi kufanya kazi za umma na kufukuzwa kwa kosa lolote.
- Maombi yaambatanishwe na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne/sita cheti cha kuzaliwa na Mafunzo ya JKT/Jeshi la Akiba kwa wanaoomba kazi ya ulinzi.
- Mwombaji aambatanishe namba ya simu kwa ajili ya mawasiliano.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni **tarehe 06/11/2023**. Usaili utafanyika **tarehe 7/11/2023 saa 2:30 asubuhi** kwenye ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale.

Maombi yatumwe kupitia anuani ifuatavyo: -

Katibu Tawala (W)

S. L. P 181

Nyang'hwale.



Kaunga Omary Amani

KATIBU TAWALA WILAYA

NYANG'HWALE.

KATIBU TAWALA WA WILAYA
NYANG'HWALE